TANGAZO LA SERIKALI Na. 684 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA KASEKESE YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kasekese ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

*Tangazo La Serikali Na. 684 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama P1 yenye majira -nukta 243689.02E, 9275350.31N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini–Mashariki katika uelekeo wa N16°07'12"E kwa umbali wa kilomita 1.06 hadi alama ya mpaka ya upimaji P2 yenye majira - nukta 243983.90E, 9276370.61N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa N54°59'55"E kwa umbali wa kilomita 1.27 hadi alama ya mpaka ya upimaji P3 yenye majira - nukta 245024.68E, 9277099.41N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S48°41'57"E kwa umbali wa kilomita 1.02 hadi alama ya mpaka ya upimaji P4 yenye majira - nukta 245791.34E, 9276425.85N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N48°48'17"E kwa umbali wa kilomita 2.09 hadi alama ya mpaka ya upimaji P5 yenye majira - nukta 244212.10E, 9275043.56N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa S59°36'39"E kwa umbali wa kilomita 0.606 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*